


Sikukuu Ya Mama

 ...Maskani, ndilo ombi langu. Bila shaka nina furaha asubuhi ya leo, kuona kufanikiwa kiroho kwa maskani hii, na jinsi ambavyo, ile ishara kule nje, wao wanajitayarisha sasa kujenga kanisa jipya. Nafikiri linahitajika. Na kuona baada...kama Bwana Yesu akikawia, baada ya sisi kuondoka, itawabidi watoto wetu kuwa na mahali pa kwenda kanisani. Nasi tunataka “kushindania imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.” Nafikiri hilo ni jambo nzuri.

² Na nilipokuwa nikija, muda mchache uliopita, kungezea kwenye shuhuda nyingi ambazo tayari zimetolewa kuhusu kuponya, katika mikutano michache iliyopita, hapa Maskanini. Daima zinalundikana, za kuponya, kuponya kukuu kwa kimiujiza.

³ Nilikuwa nimemwacha mke wangu nje, sasa hivi, na watoto m—mlangoni; na kulikuweco na dada fulani, anayeketi hapa sasa, alikuwa na furaha sana hata alikuwa analia, juu ya muujiza mkuu uliotukia juu ya mjukuu wake, kule chini, nafikiri, katika Chattanooga. Bibi Nash, hapa, mjukuu wako alikuwa anaogua ugonjwa, na kwenye mkutano wa mwisho hapa, Bwana Yesu, nafikiri, aliutambua, akasema, “BWANA ASEMA HIVI, ya kwamba, umekwisha. Naye atapata afya.” Na maskini mtoto huyo ni mzima kabisa na mwenye afya, mzima tu iwezavyo kuwa.

Na ni—ni jambo la kuchangamsha, ukisikia shuhuda hizo.

⁴ Halafu jamaa mdogo, ambaye pia yuko hapa, aliomba maombi kwa ajili ya Bibi Scotts, ambaye ndiyo kwanza afanyiwe upasuaji. Na hamu yao; mnaona, kama hakuna mtu ye yote anataka tuwaombee, kwa ninii yao...inaonyesha, mradi tu unajaribu, watu wakikutaka wewe uwaombee, wao...hamu; unaona. Wakati mwingine inakuwa mbaya sana, mpaka...si mbaya sana, bali watu wengi sana, hata inawalazimu tu kukimbia mahali fulani na kugeuza vichwa vyenu, na kujificha kidogo, mpate kuishi. Lakini, mimi—mimi nina furaha ya kwamba wao hufanya jambo hilo. Msifikiri kamwe ya kwamba mimi sipendi kuwaona, kwa maana kama wao...kama kusingekuweko na mtu aliyetaka mimi niwaombee, huduma ingekuwa wapi? Mnaona? Mnaona?

⁵ Lakini wakati mwingine wakati unaposema, “Ndugu Branham, sifahamu wakati watu wanapopiga simu namna hiyo, na—na utaenda mahali fulani.” Inanibidi kufanya hivyo kusudi nipate kuishi, kuwaombea watu. Ninyi hamninii

kamwe...Si—si mahali pamoja tu, hapa. Ni kila mahali ulimwenguni. Mnaona? Na—na inaparuzana sana. Nami nina hakika ya kwamba mnafahamu jambo hilo.

⁶ Loo, ni vizuri sana kuwa Mkristo! Sijui ningefanya nini kama si kwa ajili Kristo, na kwa hiyo...na kuwa na uhusiano na Wakristo, ambao, ni watu wa Imani ile ile ya dhamani, ambao wanamwamini Mungu na wanamtumainia; na kuamini ya kwamba siku moja yenye fahari tutamaliza vita hivi vyote, na kupata ushindi, na kusimama tumekombolewa katika mfano Wake, ng'ambo ya pili.

⁷ Halafu basi ningetaka kufanya matangazo mafupi, ya kwamba, katika kuja kwa Maskani, na kadhalika, mimi... tunafanya upya msingi wetu, hasa sana sehemu yangu kwa ajili ya zile kampeni. Kotekote katika ile mikutano, tangu nilipoanza katika jambo hili, upande wa ujilisti, miaka mingi iliyopita, hadala ya kuunda shirika fulani, kuwa na kundi lingine la watu, nilitumia tu kundi ambalo nilikuwa nimelizoea; na kutoka...na kufanya shirika fulani, ili kwamba mikutano yangu yote iendelezwe chini ya jina la Maskani ya Branham. Na hilo lingetumiwa kwenye Benki ya Union National huko New Albany, kama mahali ambapo pesa zingetumwa—kutumwa ukitumia hilo, ili kwamba zisitozwe ushuru. Kama hazikutumwa mle, nigelipia kodi pesa zote zilizochangwa, kama sikutumia Maskani ya Branham kama shirika.

⁸ Wengi wenu wamenisikia nikitangaza jambo hilo, wakati baada ya wakati. Sina budi kufanya jambo hilo, na ku... kusudi nifanye jambo hilo. Halafu basi—basi tunaanzisha shirika jipya sasa. Nasi tungetaka wote wanaojua ya kwamba mimi...Ni wangapi wamepata kunisikia nikitangaza jambo hilo, ya kwamba hesabu zote, mimi nafanya kazi kupitia kwa Maskani ya Branham? Inueni tu mikono yenu, wote... Hakika, ninyi nyote. Ni sawa.

⁹ Na kwa hiyo wakati ibada itakapokwisha, kama mkipenda, nina tamshi ndogo pale, ili kwamba ninyi, kama mtalitia sahihi mnapotoka. Ndugu Roy Roberson atalirudisha kule nyuma.

¹⁰ Maana, tutaunda shirika lingine, jambo lile lile, ili tu... lakini shirika lingine, ambamo pesa zetu zote na kadhalika, ambazo zimetolewa mikutanoni, kusudi zisitozwe kodi, zitakuwa... zitawekwa, kama kawaida, katika Benki ya Union Nationa, ipate kufanya kazi kupitia kwa Maskani, badala ya kuwa na shi—shiri...shirika lingine. Maana, hili ni shirika tayari, linaloitwa Maskani ya Branham, unaona. Na kwa hiyo kuna ya Branham fulani *hapa*, na Branham fulani *pale*, na namna hii, na mashirika mbalimbali ambayo hayaendelei vizuri sana.

¹¹ Ndugu Roberson atashughulikia jambo hilo, ninyi mnaotaka tunapotoka. Tunalithamini.

¹² Sasa, asubuhi ya leo, kabla hatujaingia katika ibada, ningetaka kusema, Bwana akipenda, ya kwamba nitajaribu kurudi tena usiku wa leo. Ninachukia kuchukua mikutano yote miwili kutoka kwa Ndugu Neville, lakini ameniomba kwa ukarimu sana kunena tena usiku wa leo. Na Bwana akipenda, nataka kuzungumza usiku huu juu ya somo la ujilisti la, linaloitwa hivi: *Ni Nani Huyu?* Unaona. *Ni Nani Huyu?*

¹³ Na kwa hiyo asubuhi ya leo, ninataka ku-. . . Nilikuwa nikifikiri juu—juu ya kunena asubuhi ya leo juu ya somo la Sikukuu ya Mama. Nami najua ya kwamba alasiri ya leo na asubuhi zimejazwa na vipindi vya Sikukuu ya Mama. Kwa hiyo nilifikiri kwa namna fulani nitaunganisha kitu fulani, kwa maana ninataka kuwaombea wagonjwa mara baada ya ibada hii kwisha, na kama kawaida.

¹⁴ Tunaamini ya kwamba Mungu ni mponya, naye huwaponya wagonjwa na wanaoteseka. Nami najua ya kwamba Yeye hufanya jambo hilo. Na ni zaidi ya ma—mashaka yo yote, jambo hilo, kwa maana kuna shuhuda nyingi kupita kiasi zilizolundikana, kwamba tunajua jambo hilo.

¹⁵ Jana nilikuwa nikiangalia kwenye gunia ambalo Ndugu Gene na Leo ndiyo kwanza waliweke, la shuhuda ambazo wamekusanya. Na lilikuwa ni gunia kubwa la miujiza dhahiri sana ya kuponya ambayo Bwana amewafanyia watu.

¹⁶ Nami nilifikiri, kama jambo hilo lingekuwa hivyo, vipi kama tungeweka hesabu ya yote ambayo yametukia? Nafikiri, katika Puerto Rico na Jamaica, peke yake, zingefikia elfu kumi, ama zaidi, shuhuda dhahiri, za kuponya kwa Bwana, ambako alifanya.

Sasa kabla hatujafungua Kitabu, hebu tuseme na Mwandishi Wake.

¹⁷ Bwana, tunashukuruni sana kwako, hiyo ni, tunapoinamisha vichwa vyetu, tunagugumiza tu maneno tusemayo; kwa maana siamini midomo ya wanadamu ina uwezo wa kueleza kujisikia kwa moyo wa mwanamume ama mwanamke, mvulana ama msichana, ambaye amepata kukugusa Wewe. Kuonyesha heshima zetu, jinsi tunavyokuabudu Wewe, na unavyomaanisha kwetu. Hilo limetutenga na dhambi, na limetutenga na ulimwengu. Na limetupa kitu ambacho ni cha Milele na kimebarikiwa. Nasi tusingepata maneno ya kutosha.

¹⁸ Kama ilivyosemwa wakati mmoja na muungwana mmoja, majuma machache yaliyopita, ya kwamba angeweza kuzungumza kwa ufasaha katika lugha kama tisa mbalimbali, akiwa na cheo cha mshauri wa Rais wetu mpendwa, Dwight Eisenhower. Na hata ingawa anaweza kuzungumza lugha tisa,

kwa ufasaha; yeye alisema, alipompokea Roho Mtakatifu, alijaribu kila tisa, wala hakuna maneno aliyoweza kupata, hakuna aliyoweza kutamka, na kwa hiyo Wewe ukampa lugha mpya kutamka na kukushukuru Wewe kwayo. Nasi tunajisikia namna hiyo, pia, Bwana; ya kwamba, wakati maisha yamekwisha, ya kwamba labda tutanena kwa lugha tofauti kabisa, ili kwamba tuweze kutamka yale tunayokuwazia Wewe.

¹⁹ Sasa tungeomba, Bwana, ya kwamba ungeibariki maskani hii, mchungaji wake, wadhamini wake, mashemasi wake, wanaoshirikiana nao wote, watu wanaozuru mahali hapa, wanaoingia na kutoka kwa milango yake. Jalia iwe daima mahali palipowekwa wakfu, ambapo waliochoka wanaweza kuingia kwenye milango yake na kupata faraja na amani nafsi mwao. Na kwamba wagonjwa wangeingia mlangoni, na kutoka wakiwa wazima, kwa sababu ya Uwepo wa daima wa Mwenyezi Mungu Ambaye anaishi chini ya dari yake.

²⁰ Tungeomba, Bwana, ya kwamba katika mpango huu unaokuja wa... ambao unafanyizwa sasa, kwamba Wewe ungekutana na ile halmashauri na wote. Na kama ikikupendeza Wewe ya kwamba kutakuwa na mwendeleo wa kumbukumbu ya maombi yaliyooombwa kwenye kidimbwi hiki cha kale, sehemu yenye magugu, siku moja; ya kwamba sasa imekuwa mnara wenye taa, kimbilio la raha kwa waliochoka, kwa sababu ya jibu la ombi hilo.

²¹ Sasa tusamehe kwa ajili ya kila kitu tulichofanya, ama kusema, ama kuwazia, ambacho ni kinyume cha mapenzi Yako; na ukumbuke, Bwana, haikutoka kwenye mioyo yetu. Labda tu lilionyesha kwa matendo yetu ama midomo yetu. Lakini, upesi, Wewe ulitusikia. Tulipoona ya kwamba sisi tumekosea, tulikuwa tayari kutubu jambo hilo. Nasi hatutaki kushikilia uovu mioyoni mwetu, ambapo tunajua ya kwamba Mungu hatayajibu maombi yetu; bali daima tukitubu makosa yetu.

²² Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba ungetubariki, asubuhi ya leo, kote kila mahali taifani, kwa kuwa ni wakati wa kusherehekea siku hii ya ukumbusho wa Sikukuu ya Mama. Lakini jalia hii isiwe tu si—sikukuu ya mama; jalia kila siku iwe namna hiyo.

²³ Mungu, jalia asubuhi ya leo, ya kwamba akina mama, wanawake, ambao wametangatanga mbali na Mungu, ya kwamba watajirudia, asubuhi ya leo, nao watatambua maana ya neno *mama*, ni “aliyezaa.” Na mama atambue ya kwamba watoto, kutokana na kuungana kwake na mumewe, wamekuwa vito vidogo vitakatifu ambavyo Mungu ameweka chini ya ulinzi wao. Halafu, Mungu atamwajibisha kwa ulezi

wa watoto hao. Na kama Maandiko yasemavyo, ya kwamba, “Mwanamke mzuri, na mama, alichu yeye, ya kwamba watoto wake watamwita mbarikiwa.”

²⁴ Ee Mungu, tunapooni siku hii, wanapoenda mbali sana na Maandiko, na kutenda karibu kama wanyama! Tunaomba, Ee Mungu, ya kwamba utatupa ufufuo wa mtindo wa kale ambao utawaita uwarudishe mahali wanapopaswa kuwa.

²⁵ Bwana, hatungeweza, kwa vyo vyote, kusahau kukushukuru kwa ajili ya mama walio halisi, kwa maana tunajua tunao wanaoishi siku hizi; mama halisi na wa kweli. Mungu, wabariki. Wao ni hazina kubwa kwetu, nasi tunaomba ya kwamba utaendelea kuwa pamoja nao, Bwana, na naomba waishi maisha yenye furaha na waone matunda ya tumbo lao la uzazi yakimtumikia Mungu.

²⁶ Na tunaomba, Mungu, ya kwamba hao wanaovaa waridi nyekundu asubuhi ya leo, ama ua jekundu, kusema ya kwamba mama zao wameaga dunia leo; naomba, Bwana Mungu, wastarehe katika amani na matendo yao yanawafuata. Tujalie, Bwana.

²⁷ Sasa litwae Neno Lako, Bwana, ukanene na watu, na ukawafariji, kwa maana hiyo ndiyo sababu tumekusanyika hapa; kuhisi Uwepo Wako, na kulisikia Neno Lako, na kubarikiwa; na kuondoka hapa tukiwa wanaume na wanawake wazuri, vijana kwa wasichana, kuliko tulivyokuwa tulipoingia. Tunaomba jambo hili katika Jina la Yesu, Mwana wa Mungu. Amina.

²⁸ Mimi napenda kusomwa kwa Neno Lake lililobarikiwa. Kwa hiyo sasa tutafungua, asubuhi ya leo, katika Kitabu cha Wakorintho wa Kwanza, na kusoma sehemu ya sura ya 15, kuanzia na ya 1.

Basi, ndugu zangu, nawaarifu ile injili niliyowahubiri; ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mnasimama,

Na kwa hiyo ninyi mnaokolewa; ikiwa ninyi mnayashika sana yale maneno niliyowahubiri; isipokuwa mliamini bure.

Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko;

Na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko.

²⁹ Mnaweza kusema, “Ndugu Branham, hilo kwa namna fulani ni fungu lisilo la kawaida kwa ujumbe wa Sikukuu ya Mama.” Vema, hiyo ni kweli. Lakini, mwajua, Mungu si wa kawaida, Naye hufanya mambo kwa njia isiyo ya kawaida.

³⁰ Nami nafikiri, yale mawazo, ya mama. Nami nina mama asubuhi ya leo, kwa neema ya Mungu, angali hapa duniani pamoja nasi. Nami ninashukuru kwa sababu ya mama. Lakini kwa kuwa ilipasa tuwe nayo, pia, ibada ya kuponya, na kwa kuwa sijui kama nitarudi tena usiku huu, lakini nilifikiri labda tungechora picha ya namna nyingine.

³¹ Mama ni mtu mashuhuri. Mwajua, wa kwanza ambaye anakupokea, katika maisha haya, ni mama yako. Hakuna mtu anayeweza kukugusa, kwa maana wewe unaanza mimbani mwake, naye anakubeba chini ya moyo wake. Naye ndiye wa kwanza kukujua, na wa kwanza kuninii, katika maisha haya, ku—kukushika. Halafu, wakati unapozaliwa, mikono yake ndiyo moja ya kwanza kukugusa na kuyapanguza majoji kutoka machoni mwako. Ndiye wa kwanza kukugusagusa na kukupenda, na kukutuliza, katika maisha haya, ni mama yako. Sasa, nafikiri hakuna heshima ya kutosha tunayoweza kumpa mama.

³² Mama ndiye wa kwanza kuwa na mtoto, naye ndiye anayehusika sana na yale mtoto huyo atakayokuwa, itategemea jinsi mama huyo anavyomwazilisha mtoto huyo katika njia ambayo hana budi kupitia. Mama ana jukumu, kutoka kwa Mungu, kumweka mtoto huyo katika njia inayofaa. Nami nafikiri hiyo ndiyo sababu mama wana mguso fulani mdogo maalum.

³³ Ninamjua mvulana fulani hapa mjini. Nafikiri mama yake yuko hapa sasa. Yeye ni karibu umri wangu. Bali sisemi jambo hili kumuudhi huyo mama; kwa maana ana maudhi ya kutosha, kama mama wote walivyo nayo. Lakini mvulana huyo hunywa pombe, naye ni mlevi sana. Basi wakati anapolewa sana, yeye atakuja nyumbani na kuruka kitandani pamoja na mamaye na kumkumbatia. Naye ana wajukuu. Lakini kuna kitu fulani juu kupapaswapapaswa na mama, ambacho huonekana kama kinachukua mahali tofauti na kitu kingine cho chote kinachoweza kugusa; hiyo ni, katika maisha haya, tukinena kibinadamu.

³⁴ Mnajua, mtu kama Musa, yeye. . . Kama ninaweza kusifu cho chote katika tabia yake, ilikuwa ni kwa sababu alikuwa na mama aliyetumwa na Mungu. Unajua ndiye aliyekuwa ameomba, Yokebedi, naye alikuwa ametamani sana kumpata mtoto huyu. Na wakati alipozaliwa, yeye ndiye aliyemtuliza, na kumkumbatia kifiani na kumjengea kisafina na kumweka kwenye manyasi, wakati maskini moyo wake ulikuwa unavunjika. Mtoto wake mchanga wa pekee, na alikuwa m—mtoto mashuhuri kuliko wote waliokuwako ulimwenguni. Na jinsi mama anavyompenda mtoto ye yote! Lakini kuona mtoto huyu mashuhuri mdogo.

³⁵ Halafu basi, moyoni mwake, mama alijua ya kwamba huyu alizaliwa kwa kusudi fulani, halafu anamchukua na kumweka

katika makao ya mamba, huko mtoni. Kwa imani yeye alifanya jambo hilo, akijua ya kwamba Mungu aliweza kumshughulikia; na kufanya mhitasari wa upendo wa mama, na matendo ya tabia ya imani yake. Kwa kuwa imani haijiweki juu ya mchanga unaosogea wa yale inayoweza kuona; imani inatulia kwa uchaji juu ya mwamba usiosogea wa Neno la Milele la Mungu. “Kwa kuwa kwa imani,” yasema Maandiko, “alifanya jambo hili.”

³⁶ Nayo imani inaweza kuchukua msimamo wake juu ya mwamba, ambao mawimbi yanapiga msingi wake, na kuangalia moja kwa moja kwenye uso wa mauti na kujua ya kwamba itakuwa tu muda kidogo, lakini imani inaweza kuangalia upande wa pili wa bahari kumwona Yeye aliyesema, “Mimi Ndimi ufufuo na Uzima,” na kukosa kusikia hata hayo mawimbi yakipigapiga kwa nguvu.

³⁷ Hiyo ndiyo imani ambayo mama ya Musa alikuwa nayo. Yeye alimfundisha na kumlea katika nyumba ya kifalme ya Farao, akimfundisha ya kwamba alizaliwa kwa kusudi fulani, ya kwamba Yehova alikuwa amejibu ombi lake. Na, yeye...yeye asingaliweza kuwa na mwalimu bora zaidi. Hilo ndilo lililosaidia kuunda tabia aliyokuwa nayo Musa.

³⁸ Ninaamini ilikuwa ni Abraham Lincoln ambaye wakati mmoja alitoa tamshi kama hili... .

³⁹ Sasa, mimi si wa chama cha Democrat wala cha Republican, mimi ni ninii tu...Mimi ni Mkristo. Kwa kuwa, nafikiri upande mmoja haungeweza kusema neno juu ya upande huo mwingine; pande zote ni ufisadi tu. Lakini, Abraham Lincoln, kwa mawazo yangu, alikuwa mmoja wa...na alikuwa mmoja wa raisi wakuu sana ambao Marekani hii imepata kuwa nao; akiweko Washington, na kadhalika.

⁴⁰ Kwa kuwa, Abraham Lincoln alikuwa a—alianza vibaya. Alikuwa maskini. Hakuwa na msingi, tuginena juu ya elimu, ama—ama kitu fulani kikuu, ama pesa, ama kitu fulani ambacho kingemsaidia, kama alivyofanya Washington. Washington alikuwa amehitimu chuoni, na a—alijua; alikuwa mtu mwenye akili, mtu mashuhuri, kwanza. Lakini Lincoln alilelewa kwenye kibanda kidogo cha magogo, chini ya nchi kuu ya Kentucky, bila sakafu; katika kibanda kidogo cha kale cha magogo, ambacho kimewekwa kama kumbukumbu hapa Louisville sasa. Lakini, kwa kuwa alikuwa mtu mashuhuri, na ilimbidi kujifunza kuandika, kwenye shamba alilolima, kupanda mahindi.

⁴¹ Lakini huenda nikawaambia vijana jambo hili. Hivi mnajua Abraham Lincoln hakuwa na kitabu maishani mwake, mpaka baada ya umri wa miaka ishini na mmoja, ila Biblia na

kitabu cha wafia imani cha Fox? Mnaona, unachosoma ndicho kinachoifanya tabia uliyo nayo. Si ajabu tuna kundi la watu wasioweza kujizuia leo; magazeti madogo ya kale ya hadithi za kujibunia, machafu na ya kipuuzi, yanawekwa kwenye vibanda vya kuuzia magazeti. Yeye alikuwa na Biblia na kitabu cha wafia imani cha Fox. Angalia kile vilivyomfanyia!

⁴² Lakini mbele ya mambo hayo yote, siku moja alitoa tamshi kama hili. Akasema, “Kama jambo zuri lingeonekana kwangu, ni kwa sababu ya mama mcha Mungu,” ambaye alimlea apate kumtumikia Bwana.

⁴³ Mnaona, mtoto humsikiliza mamaye; mguso mdogo kuhusu mama huyo, ambao mtoto atasikiliza. Wakati ameudhiwa, atamwendea mama apate faraja kabla hajamwendea baba. Kwa sababu, yeye ndiye aliyetangulia kuwa naye, mwajua. Na kuna kipawa ambacho Mungu humpa mama, kuwa namna hiyo; ninamaanisha mama halisi. Sasa, ninaamini ya kwamba mama ni waadilifu na wacha Mungu.

⁴⁴ Lakini ninaamini, Sikukuu ya Mama, kama hii, ni jama, kupata pesa nyingi sana kutokana na maua na kadhalika. Lakini siku ya mama inapaswa kuwa ni kila siku. Si ati kumtumia shada la maua kwenye Sikukuu ya Mama, bali kumpenda na kumshughulikia siku mia tatu na sitini na tano usiku na mchana, mwaka mzima. Lakini, bila shaka, ulimwengu wa biashara umeshika mambo kama haya sana, na jambo hilo lina—lina—linamvunjia mama heshima.

“Loo, vema, Sikukuu ya Mama ya mwaka jana nilimtumia shada la maua.”

⁴⁵ Yeye angefurahia, zaidi sana, kuketi tu na kuzungumza naye kidogo tu, kumwandikia barua mstari mmoja, kumpigapiga begani, kumbusu shavuni, umwambie unampenda. Litaenda mbali zaidi kuliko maua yote ambayo ungeweza kununua kutoka kwa mwuzaji maua. Hiyo ni kweli.

⁴⁶ Ninaamini ilikuwa katika zile Amri Kumi, hayati Cecil DeMille, ambaye aliandika na kuweka kwenye sinema moja ya sinema zilizo nzuri kuliko zote katika ulimwengu wa sinema. Na kabla haijaonyeshwa watu, ama kusambazwa, Cecil DeMille alimwalika Oral Roberts na Demos Shakarian, na kundi la wahudumu wa Injili yote, akawapeleka kwenye studio yake mwenyewe na kuwaonyesha ile sinema ya Amri Kumi inayochukua muda wa masaa manne, na kuwauliza maoni yao juu yake. Mungu na aipe raha nafsi yake shujaa!

⁴⁷ Nami nilipoiona, nilikuwa nikiiangalia, na kamwe sijasahau tamshi fulani dogo. Kama ye yote wenu alipata kuonia, ilikuwa ni wakati binti wa Farao. . . baada ya Musa kujua ya kwamba yeye a—alikuwa Mwebrania, naye alikuwa ameamua kwenda akaishi pamoja na watu wake. Basi hapa

aliketiki mama yake ambaye siku moja alikuwa mrembo, amefifia, mwenye nywele zenye mvi na uso wenye makunyanzi, huku ameketi kwenye kiti chenye mikono kilichochakaa; mama halisi. Naye binti wa Farao akaingia. Naye akasema, “Mimi ni mtoto wa nani, hata hivyo?”

⁴⁸ Na wakati jambo hilo liliwekwa wazi, ya kwamba Yakobedi alikuwa ndiye mama yake halisi. Binti ya Farao, huku amejipodaa na kadhalika, na amejipamba kwelikweli; alisema, “Lakini, angalia! Huenda yeye akawa ni mwanao, lakini,” akasema, “nilimpa utajiri na fahari. Wewe usingeweza kumpa kitu ila mashimo ya matope.”

⁴⁹ Lakini yule mama mzee mwenye mvi akasema, “Lakini mimi nilimpa uhai.” Hilo ndilo linaloleta tofauti. “Nilimpa uhai.” Mungu akampa Uzima wa Milele. Ni kweli kabisa, mama!

⁵⁰ Wakati mwingine watu huniambia, zaidi sana katika kampeni zangu, mimi “daima ninahubiri juu ya ufufuo.” Nami nilisoma somo asubuhi ya leo, sura ya 15 na aya ya 4 ya Wakorintho wa Kwanza, juu ya ufufuo.

⁵¹ Bali, mnaona, jinsi wanavyomweka mama siku hizi, ni nyungu ya maua iliyowekwa kando ya bibi mkongwe, ambaye ni mkongwe sana hawezi kuamka, labda, mnyonge, mwenye mvi kichwani, na mwenye makunyanzi, huku ameketi kwenye kiti chenye mikono. Hiyo ni kweli kabisa. Bali ninataka kuchukua somo langu na kuchora picha nyingine ya jinsi mama alivyo.

⁵² Mtu fulani alisema, “Unahubiri sana kupita kiasi juu ya ufufuo. Karibu kila Ujumbe una kitu fulani kuhusu ufufuo.”

⁵³ Mbona, hakika. Huo ndio kiini cha msingi halisi wa Injili. Haidhuru Yeye alifanya nini, kama Yeye hakufufuka katika wafu, basi hayo yote yalikuwa bure. Hiyo, kwangu mimi, inathibitisha ya kwamba Yeye ni Mungu. Inathibitisha kila dai alilofanya; ule ufufuo! Na pia ni mahali pa kustarehe kwa nafsi. Huo ndio mwanzo. Huo ndio kilele cha faraja yetu.

⁵⁴ Na wakati tunapooa ya kwamba Yeye alifufuka katika wafu, hilo linatuweka mahali petu, na silaha ya Injili, vitani, kupigana vita. Kwa kuwa, tunajua ya kwamba Yeye alisema, “Yeye atakayeyapoteza maisha yake kwa ajili Yangu atayaokoa tena.”

⁵⁵ Nami nafikiri ndio—ndio kilele kikuu cha Injili Kamili, ni ufufuo, na ahadi zake za Kiungu, na faraja inayowapa hao wanaoitumainia. Kwa kuwa, unaahidi ule muungano mkuu wa kuungana kwetu pamoja tena. Unaahidi, na—na kutoweka kwa dhambi yote. Unaahidi na kutoweka kwa ulemavu wote, na mateso yote ambayo tumepata katika jambo hili,

yaliyotulazimu kupitia, katika maisha haya. Unaahidi, na kutoweka kwa yote hayo. Unaahidi hata mauti yatashindwa kushikilia, nasi tutafufuka katika mfano wa Yesu. Kwa hiyo, kwa maoni yangu, ufufuo ndio ahadi kubwa kuliko zote katika Maandiko. Hapo ndipo umetiwa muhuri.

⁵⁶ Na ile Pasaka ya mwisho, nilipokuwa ninahubiri juu ya mambo matano ya:

Maishani, alinipenda; kifoni, akaniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali sana dhambi
zangu;
Lakini, alipofufuka, alinihesabia haki milele.

⁵⁷ Hiyo ndiyo Siku yangu, hiyo Siku kuu ya siku! Na kuona kile yote yanamaanisha, kwetu sote, katika ufufuo, tunapofanya kazi na kuingojea Siku ile iliyobarikiwa kuliko siku zote!

⁵⁸ Inatupa ahadi ya kwamba siku moja hawa mama wazee, waliodhoofika, wanyonge, wenye mvi kichwani, na waliovunjika moyo watabadilishwa. Si kwamba tu mama ataketi pale, peke yake, bali jamaa yake yote pamoja naye.

⁵⁹ Na hiyo itakuwa ni siku ya namna gani! Utakuwa ni wakati wa namna gani, tutakapoziangalia nyuso za hao waliotupenda sana! Jinsi itakavyoleta tofauti asubuhi hiyo, wakati tutakapowaona wapendwa wetu, na—na kuangalia jinsi watakavyokuwa wakati huo! Mateso yote yataondolewa. Uharibifu wote wa mateso utakwisha. Hakuna tena mashavu meupe ya mauti. Hakuna tena majozzi kutoka machoni. Ufufuo unaahidi mambo haya yote. Hakutakuweko na mazishi tena. Hakuna kugusagusa mtoto mashavuni tena, ambaye ni kama kipande cha mawe; ambapo mzishi amemia dawa asioze, na kusukumwa na kupakwa rangi, na kadhalika, kuonekana wa kawaida. Hilo halitahitajika tena, kule.

⁶⁰ Halafu ninafikiria juu ya hao wakisimama kule, wapendwa wetu, mama zetu, jamii zetu, rafiki zetu wote; na kuwaona katika miili yao isiyopatikana na mauti, miili yao ya kiungu; tukiangalia tabia zao, kuona jinsi wanavyotenda kwa utamu na utulivu, hakuna tena kushikwa na wasiwasi wala shida. Kuwaona wamesimama katika mfano wa Bwana Yesu, hiyo itakuwa siku nzuri sana.

⁶¹ Na kila mmoja wetu, katika nia zetu, anatarajia na kutamani saa hiyo ya faraja, tutakapokutana nao. Kila mmoja anafikiri juu ya mpendwa wake, labda mama yao aliyeaga dunia. Basi itakuwa siku ya namna gani, utakapomwona tena! Na kwa baba, na kwa ndugu, na kwa...wapendwa wote, itakuwa siku ya namna gani!

⁶² Ninafikiri, pia, sasa hivi. Ninafikiria juu ya jamaa yangu, itakavyoamaanisha kwangu Siku hiyo.

⁶³ Ninafikiri ya kwamba, kwenye asubuhi hiyo ya ufufuo, labda wa kwanza atakayekuwa kunilaki atakuwa mtoto wangu mdogo Sharon. La, hatakuwa akitetemeka. Ibilisi huyo hawezi kuingia mahali pale. Hakuna pepopunda anayeweza kumgusa katika Nchi hiyo. Hatakuwa akiniaga kwaheri. Macho hayo madogo ya bluu yatakuwa yakicheza anapoitupa mikono yake na kulia, “Baba!” Nitafurahiwa kumwona, kujua ya kwamba yeye hatakuwa tena; kujua ya kwamba yote imekwisha, ndiyo sababu ninahubiri ufufuo kwa nguvu sana.

⁶⁴ Ndipo nitamwona mama yake, mama ya Billy, mtoto wangu. Nami nina kumbukumbu nyingi sana papo hapo zilizodumu siku nyingi. Ninakumbuka wakati nilipokuwa nikimchukua, au Bw. Combs, hapa, alipokuwa akimchukua akabebwe mara ya mwisho, nami nilikuwa ninamfuata, katika gari. Tulipokuwa kwenye Barabara ya Saba, pale pale; Billy, mwenye umri wa miezi kumi na minane.

⁶⁵ Jinsi wangemleta barabarani, na kumwacha mama amwone. Naye angelala pale na kulia, na kumwangali mtoto wake, bali hageweza kumkaribia.

⁶⁶ Na halafu alipokuwa akishuka barabarani, huyo mzishi alikuja na kushuka kwenye—kwenye—kwenye Barabara ya Saba. Mama hapa alikuwa anamshughulikia wakati huo. Naye alikuwa amesimama huko nje uwanjani, na suruali yake ndogo na fupi, na kofia ndogo nyekundu iliyovutwa upande mmoja kichwani mwake. Na wakati mama huyo, akiwa amelala kwenye machela hayo, nyuma ya gari la kubebea wagonjwa, akiniangalia, alipomwona mtoto wake mchanga amesimama uwanjani, akijua amepanda gari kwa mara yake ya mwisho; aliamka kwenye machela na kupiga kiyowe, akatoa mkono wake uliokonda sana, apate kumkubatia mtoto wake mchanga huko uwanjani. Bali hangeweza kumshika.

⁶⁷ Loo, itakuwa furaha kumwona siku hiyo. La, hatakuwa na mikono iliyokonda, wala hayo mashavu hayatakuwa yamedidimia. Lakini atasimama katika uzuri wa kimbinguni wa malkia wa Mbinguni, na wa mama. Macho yake meusi, meusi kama mabawa ya kunguru, yatakuwa yakicheza-cheza kwa furaha. Yeye hatakuwa ameinama; ambapo, huyo Ibilisi wa TB kamwe hataingia kwenye Nchi ile. Bali, atasimama katika uwepo Wake, asiyepatikana na mauti.

⁶⁸ Nafikiri, basi, wa pili kuja kunilaki atakuwa ni Edward, ambaye tulimwita “Humpy,” kwa jina la mkato. Yeye alikuwa wa kwanza kwenye ule mnyororo wa viungo tisa vya mnyororo wa jamaa ya Branham. Ndiye aliyekuwa kiungo cha kwanza kuvunjika; ndiye aliyenifuata. Nitamwona Edward akinikimbilia. Hata hivyo alikufa akali mvulana, mwenye umri

wa miaka kumi na tisa. Nami nitakapomshika mkono, nina hakika tutakuwa na mambo mengi sana ya kuzungumzia, ya ujana, kwa kuwa tulikuwa marafiki sana. Tulikaa pamoja. Aliniruhusu kuvaa suti zake, na—na—kadhalika, kama ndugu halisi walivyofanya. Itakuwa furaha kumwona tena.

⁶⁹ Nami nitamsikia akisema kitu kama hiki, “Ulipata habari yangu, Bill? Ulikuwa unafanya kazi kwenye ranchi ya ng’ombe, wakati wa kuaga kwangu dunia. Lakini nilipokuwa hospitalini, nilituma habari, ‘Mwambie Bill kila kitu ni shwari.’”

Nitafurahia kusema, “Naam, nilipata habari, huko mbugani.”

⁷⁰ Halafu, nakisia, atakayefuata atakuwa Baba yangu. Ndiye kiungo kilichoaga dunia baadaye, na . . . La.

⁷¹ Nafikiri Charles ndiye kiungo kilichofuata, ndugu yangu mdogo. Alipata ajali ya motokaa akali mvulana mdogo tu. Daima alikokota mguu wake wa kuume, alipotembea. Lakini, mwajua, nitakapomwona, yeye hatakuwa unaukokota mguu huo. Yote yatakuwa yameisha, atasimama katika uzuri wa kijana mwanamume.

⁷² Naye ataniambia, kitu kama hiki, huku anatambasamu. Atasema, “Naam, Bill, hakuna ajali huku juu. Ninakumbuka ule usiku miliopata ajali ya motokaa, ulinizungumzia, huku umesimama kwenye tao la nyumba yetu ndogo,” nami ninaangalia juu yake, sasa hivi. “Ulinizungumzia juu ya Bwana, masaa machache tu kabla sijaaga dunia. Nawe ulikuwa mimbarani nilipoaga dunia.”

⁷³ Ndipo baba atakuja. Loo, ninaweza kumwona. Ingawa alinicharaza viboko sana, vile hasa nilivyohitaji, bali nitaona lile vunga la nywele za mawimbiwimbi, zinang’aa sana kuliko zamani, kwenye siku ile. Naye ataniangalia, na kusema, “Mvulana wangu, wajua, Baba kamwe hataondoka mezani hapa, tena, akiwa na njaa, kusudi watoto wake wapate chakula, kwa maana hapa tuna kingi. Hakuna upungufu hapa.”

⁷⁴ Kumwona wakati yeye anafanya kazi, akipata ujira wa senti hamsini ama sabini na tano kwa siku, halafu anaondoka mezani kusudi watoto waweze kula, anarudi kazini tena. Naye alifanya kazi kwa bidii sana hata shati lake lingechomwa na jua mgongoni, naye mama angelikata kwa makazi.

⁷⁵ Nitamsikia akisema kitu kama hiki, “Bill, unakumbuka usiku ule wewe na Ndugu George mlikuwa kuniombea nilipokuwa ninaaga dunia? Unajua, milimwambia mama ya kwamba kulikuwako na Malaika wawili waliosimama kitandani, na malaika mwekundu miguuni. Naye huyo

malaika mwekundu alikuwa akijaribu kunichukua, bali yule Malaika mweupe akasimama kati. Hatimaye walinipeleka Nyumbani.

⁷⁶ Halafu, pia, mwingine kwenye kiungo aliyeaga dunia, ama aliyeondoka, atakuja Howard. Nitamwona Howard; jinsi tulivyotembea nchini, kila mahali; alitwa kuwa mhudumu; mtu wa kupendeza sana, bali marafiki wake wakamzuia. Mazungumzo ya mwisho niliyozungumza naye, alisema, “Nitakapoaga dunia, Bill. . .”

⁷⁷ Ni—nilimwona akiaga dunia, kwa ono, kama miaka minne kabla hajaondoka. Nikamwambia nilimwona Baba akitayarisha kaburi lake na kusema ndiye atakayefuata.

⁷⁸ Naye akasema, “Kuna jambo moja ninalotaka unifanyie.” Akasema, “Nimeyaharibu maisha yangu. Nimeoa na kila kitu. Si—sijui kumetukia nini.”

Nikasema, “Hivi unamwamini Yeye, Howard?”

⁷⁹ Akasema, “Kwa yote yaliyo ndani yangu, ninamwamini Yeye.” Yapata siku mbili au tatu kabla hajaondoka, alinyosha mambo na Mungu, na Ndugu Neville na hao wengine kule. Naye akasema, “Kuna jambo moja minalokutaka ufanye. Nitakapoaga dunia, Bill, hebu waniimbie, *‘Yeye Ataelewa, Na Kusema, ‘Umefanya Vema.’*”

⁸⁰ Ninaamini, kabla sijampa Howard mkono, nitamsikia akisimama na kuniangalia, na kusema, “Bill, Yeye alielewa.”

⁸¹ Baadaye, watakuja Ndugu Seward, Ndugu Frank Broy, Ndugu George DeArk. Loo, ufufuo unamaanisha mengi kwangu. Ninaitazia kwa hamu saa ile muhimu ya kutiwa taji. Na wakati ile Nuru itakapoanza kuenea, “Tutajua kama tunavyojuliwa.” Tutafahamu, na—na tutawakumbuka marafiki wetu na wa—wale wamekuwa kule.

⁸² Na—na wengi, kutakuweko na wengi kule ambao hata hatukufikiri hata wangukuwa kule. Kwa kuwa, mwajua, ni katika wakati huo, ambapo ninaamini ya kwamba “ule mkate tulioutupa kwenye maji ya kibinadamu yenye usumbufu, utaturudia kwenye Siku hiyo.” Tutakapoona matokeo ya ushuhuda wetu, katika watu ambao hatukufahamu waliyotenda Kwake, labda watakuwa kule. Itakuwa Siku ya namna gani!

⁸³ Halafu, pia, mbegu tulizopanda, bila hata kufikiria zitakavyofanya, lakini hizi hapa. Zilizaa matunda ya thamani, nasi tutawaona katika Siku hiyo, marafiki wakaidi na jamii zetu.

⁸⁴ Nami nafikiri juu ya maelfu niliowaona wameongoka, naam, wamefikia milioni kadha sasa, wakienda, na jinsi

huduma yao ilivyokuwa. Loo, itahitaji zaidi ya ufufuo. Itachukua Umilele, kuzunguka, tukipeana mikono na kutafuta kujua mambo nisiyojua sasa.

⁸⁵ Kutakuweco na hao mama wenye mvi, ambao mnavaa hayo maua meupe kwa ajili yao leo, ambao watawaona, nao watakuwa na sura nzuri. Si wakiwakilishwa na nyungu ya maua, ama picha ya kizee chenye mvi; bali katika mfano na uzuri wa ufufuo, wao watasimama katika mfano wa Kristo, miili yao ya kimbinguni, wakiwa vijana na warembo milele. Hakika, hiyo ndiyo raha. Hiyo ndiyo Sikukuu ya mama ninayongojea. Huko ndiko kuvikwa taji. Si kutia ua kotini, bali kutiwa taji kwa nafsi, kwa kuwa Mungu amembadilisha!

⁸⁶ Nawazia juu ya mama yangu mzee, akiwa mzee na amedhoofika, anatemeka kwa upooza. Hatakuwa akifanya hivyo Siku hiyo. Itakuwa tofauti wakati huo. Na Nuru hiyo kuu itaanza kuenea, tutakapoanza kuangalia kila mahali, na ile duara kuu itakuwa ikipanuka, na kupanuka, na kupanuka. Yote inarudisha tu nuru ya kukaribia kwa Yesu. “Na baada ya kitambo kidogo,” kama ulivyosema ule wimbo, “nami nitamwona Yesu hatimaye.”

Atakuwa akiningojea,
 Yesu aliye mwema sana na wa kweli,
 Kwenye Kiti Chake cha Enzi, Yeye
 atanikaribisha Nyumbani
 Baada ya siku hii kwisha.

⁸⁷ Halafu tutakapomwona, na hatutakuwa kama tulivyo sasa. Tuta-tutajua jinsi ya kumpenda Yeye zaidi. Hatutasimama nyuma na woga mdogo; kwa sababu, tutakuwa kama Yeye. Vema, Yeye atakwua wa jamaa yetu zaidi ya alivyo sasa. Tutamfahamu vizuri zaidi. Kwa sababu, tuko mbali sana, katika hii miili ipatikanayo na mauti; wakati huo tutakuwa na mwili kama mwili Wake wenye utukufu. Tutajua jinsi ya kumwabudu. Nasi tutakapoona yale Uwepo wa Utu Wake umetufanyia, ukatubadilisha; ule mzee ukawa kijana, na wote waliolemaa wakanyoshwa. Loo! Tutafahamu wakati huo ni kwa nini nguvu Zake zilituponya.

⁸⁸ Maswali ambayo yamekuwa moyoni mwetu, “Yeye anawezaje kufanya jambo hilo? Ni kitu gani kingefanya jambo *hili*?” Kwa vyo vyote, kwa njia za ajabu, yatatoweka. Vile vifundo vilivyofungwa nyuma niani mwetu, “Itakuwa hii? Ingewezekanaje?” Kwa njia moja, au nyingine, vidole vitukufu vitafungua tu, vitafungua vifundo hivyo, na kuvifafanua, na yote yataishia kwenye taji moja kubwa ya upendo.

⁸⁹ Ndipo tutamwona Yeye. Ndipo tutakuwa kama Yeye. Ndipo tutamwabudu. Ndipo tutakapomwona mama jinsi Mungu anavyomtaka.

Mama hangekamilika Kule bila jamaa yake.

⁹⁰ Bila shaka, wakati mkuu sana wa maisha yake yote ni kuwaona watoto mezani, na wote wakiwa wenye afya na furaha; na—na—na kumwona akitia kahawa, ama lo lote lile analofanya, na kupika chakula cha jioni, naye pamoja na baba wanaketi chini. Mbona, huo ndio wakati wa furaha sana katika maisha ya mama, kuwaona watoto wake wote wakiwa nyumbani.

⁹¹ Sasa, usikose, sijie ukaikosa Siku hiyo. Hebu ule mnyororo mkuu wa jamaa yako ushikamanishwe pamoja, kiungo kwa kiungo. Hebu kila taruma iwe kwenye gurundumu. Ndipo tutakapoketi pamoja na jamaa zetu na katika makundi, katika chandalua cha Milele, itakuwa siku ya namna gani! Ndipo tutafahamu.

⁹² Ndiye aliyehidi jambo hili, katika Ufunuo 1, ambapo ilisema, ya kwamba, “Upanga mkali ukatao kuwili ulitoka kinywani Mwake.” “Aliitwa Neno la Mungu.” Na ni kutoka kwenye mdomo ule ule, ambapo alisema, “Mimi Ndimi niliye hai, ambaye nilikuwa nimekufa; na ni hai hata milele na milele.” Kutoka kwenye mdomo ule ule, katika Yohana 6, thelathi- . . . inasema hivi, ya kwamba, “Sitampoteza ye yote, bali nitamfufua tena katika siku za mwisho.” Ndiye aliyetoa ahadi; mdomo iuo huo wa thamani. Ndiye anayetuokoa, Ndiye atuponyaye, Ndiye aliyetukomboa, na Ndiye atakayetufufua katika siku ya mwisho.

⁹³ Kama wewe ndiye kiungo hicho dhaifu ambacho kimeutenganisha muungano huu mkuu wa jamaa kwenye Siku ile, naomba Mungu wa Mbinguni, asubuhi ya leo, kwa namna fulani katika njia ya ajabu, avifungue hivyo vifundo vidogo vilivyofungwa moyoni mwako, na akufunulia upendo alio nao kwako, na naomba uje kwa utamu ukamtumikie Yeye.

Tunapowazia nambo haya, na tuombe.

⁹⁴ Kabla tu hatujaomba, nanyi mmeinamisha vichwa vyenu, nitawaomba. Je! mngetaka, kwenye Sikukuu hii ya Mama, kuyaweka maisha yenu wakfu tena Kwake, tukiutarajia ufufuo ule? Mngeweza kumwinulia mikono yenu? Huku kila mmoja . . . Mungu awabariki.

⁹⁵ Kungekuwako na mwenye dhambi aliyeko sasa, angesema, “Ee Mungu, mimi sijajishikiza kwenye mnyororo ule. Mimi ndimi nitakayekosekana wakati mama atakapoanza kuangalia kila mahali Utukufuni. Sitakuweko, kwa kuwa bado sijafanya amani yangu na Mungu. Sina tumaini la Uzima wa Milele ndani yangu. Lakini leo ni—ninataka kufanya hivyo?” Ungeweza kuinua mkono wako, useme, “Niombe, Ndugu Branham, wakati huu. Nataka kukumbukwa katika maombi, kwa maana nina wapendwa wangu huko ng’ambu ya bahari, bahari ya Uzima, nami nataka kuwalaki”? Inueni mikono yenu.

⁹⁶ Ama mtu fulani ambaye amerudi nyuma, naye angetaka kurudi leo, na kusema, “Bwana, ninajiweka wakfu tena Kwako; ninakuja kufanya upya agano langu pamoja Nawe,” mngeweza kuinua mikono yenu?

⁹⁷ Baba yetu wa Mbinguni, inapokaribia, siku hii itafanya siku moja karibu zaidi na lile tukio kuu. Na tumelazimishwa tu, kila mwaka, kuona jambo hili likiwakilishwa.

⁹⁸ Kama vile watu walikuwa wakipanda kwenda Yerusalemu kwenye Siku ya Pentekoste, na kwa ajili ya kutakaswa kwo lile sanduku na madhabahu, na—na kwa ajili ya kutoa sadaka ya dhambi; kila mwaka wao walikumbushwa, wakati huyo mwana-kondoo alipokufa huko nje, ya kwamba wakati ungefika ambapo Mwana-Kondoo wa Mungu angeuawa, kuondolea mbali dhambi. Kila wakati huyo jamaa mdogo alipolia, nayo damu ikanyunyiziwa mikononi mwao, wao walikumbushwa ya kwamba wakati unakuja ambapo angetokea Mwana-Kondoo wa Mungu, ambaye angelia, “Eli, lama . . . ? Eli, lama . . . ?” msalabani.

⁹⁹ Majuma machache yaliyopita, kabla sijaondoka kwenda katika utumishi Wako, kule California, hii Indiana ilikuwa tupu na imekufa, wala hakukuweco na uhai, kama ilivyoonekana. Maua yaliyokufa katika msimu uliopita wa kupukutika majani. Majani yalikuwa yametoka mitini. Nao utomvu mitini ulikuwa umeingia kwenye mizizi, na kila kitu kilikuwa kimekufa.

¹⁰⁰ Lakini kulikuwako na msimu ambapo jua lilianza kuangaza kwa njia tofauti. Jua lile lile liliangaza katika msimu wa kipupwe, lakini mbingu zilikuwa zimebadilika na jua likaangaza vinginevyo. Nalo jua lilipowaka, pamoja na vitu vya duniani, uhai ulitota, kila mahali. Majani yakirudi mitini. Kuondoka . . . Uhai uliokuwa umeondoka kwenye jani, nalo hilo jani likapukutika, bali huo uhai uliingia ardhini; ukarudi katika uzuri mpya, katika uzuri wa ujana. Ua lililokuwa limetoa harufu yake, lililokuwa limetoa uzuri wake unaong’aa na kuanguka ardhini; lilizaliwa, likachipuka tena katika ujana wake, likiwa na harufu mpya.


Tunakumbushwa jambo gani, Bwana, kwenye masaa haya?

¹⁰¹ Nao ulimwengu umetoka kuwa jangwa lenye ukiwa na lililo tupu, likawa paradiso ya uzuri, na nyuki na ndege wanaimba, na kila kitu kina furaha, na miti inacheza-cheza katika pepo za joto la msimu wa kuchanua. Joto na furaha zilikuwa ardhini tena, kwa sababu ya jua, j-u-a.

¹⁰² Bali siku moja M-w-a-n-a atakuja na mabawa Yake yenye kuponya, na uhai huo mdogo uliofichwa kama utomvu mtini, ardhini, kama u—uhai ulio kwenye mbeu ya ua, utachipuka upya tena, usikauke tena. Loo, jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hili!

¹⁰³ Na kulikuwako na mikono mingi, mingi sana iliyoinuliwa asubuhi ya leo, kwa maana wao wanajua ya kwamba ng'ambo ya pazia kule, kuna kitu fulani. Wao wanatamani sana kumwona mama. Wanatamani sana kuwaona wapendwa wao na rafiki zao, na kujua siri hizi zote, jinsi walivyokuja hapa, na kote katika wakati. Yote yako nyuma ya pazia lililofichwa. Na siku moja Wewe unakuja. Nao waliinua mikono yao; wao—wao—wao—wao wanataka kuwa na hakika, Bwana. Wao wanajifanya upya tena, nami vivyo hivyo. Sasa tusaidie, Bwana. Ifanye mpya imani yetu na nguvu zetu.

¹⁰⁴ Na tunapohisi kule kukaribia kwa Bwana. Na miaka hamsini iliyopita, kulitokea pentekoste mpya duniani. Roho alianza kufunua mambo. Nasi hapa kwenye ishara ya mwisho, kabla tu ya kule Kuja. Tunajua kule kukaribia kwa Bwana ku karibu. Nasi tunaona wagonjwa wakiponywa magonjwa yao, jambo ambalo limekuwa la kisiri kwa ulimwengu, kwa miaka elfu mbili, tangu wale mitume. Lakini hapa linatukia tena, manabii wakiinuka, Malaika wanatokea, ishara na maajabu. Ni kitu gani? Ufufuo unakaribia. M-w-a-n-a anakuja.

¹⁰⁵ Na tuwe tayari, Bwana. Na tuikumbatie kila ahadi ya Kiungu; usifikirie juu ya vifundo hivi vidogo vilivyokusanywa na sayansi, na kadhalika, ya kwamba jambo hilo haliwezi kutukia. Naomba waanze kufungua, asubuhi ya leo, kwa ninii ya Kiungu. . . [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] . . wakati Yeye anapopitia kwenye Maneno ya Biblia ya Mungu, kama ala ya muziki yenye ulinganifu wa sauti, kuimba wimbo, “Mimi Ndimi niliyekuwa nimekufa, na ni hai milele na milele.” “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona.” “Kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” “Na itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, ya kwamba nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; ishara na maajabu; wazee wataota ndoto, na vijana wanaume wataona maono,” ishara za mvua ya vuli na za wakati wa mwisho. Na isikike kati yetu, asubuhi ya leo, Bwana, na jalia imani yetu iwe yakini. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina. 

Sikukuu Ya Mama, Vol. 8 No. 7
(*Mother's Day*, Vol. 25 No. 1)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Mei 10, 1959, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1996 na Voice Of God Recordings.

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

Copyright notice

All rights reserved. This book may be printed on a home printer for personal use or to be given out, free of charge, as a tool to spread the Gospel of Jesus Christ. This book cannot be sold, reproduced on a large scale, posted on any website other than www.branham.org, stored in a retrieval system, translated into other languages, or used for soliciting funds without the express written permission of Voice Of God Recordings®.

For more information or for other available material, please contact:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org